# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org    redazioneasc@adoratrici-asc.org

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru

5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 8, Septemba 2019


Mhariri


## Upendo ni shukrani

Mwandishi mkubwa wa Kilatino na mwanahistoria Tacitus aliwahi kuandika: “Shukrani ni kumbukumbu ya moyo.”

Dini nyingi na tamaduni nyingi hutambua hisia hii kama tunu na, mimi binafsi, mara nyingi nilizingatia hilo, kwa sababu niliiona daima kwamba ni ya hiari, lakini pia ni heshima, kujibu kwa shukrani kwa kila tendo au ishara ya umakini au msaada unaopokelewa. Walakini ilikuwa wakati wa mazungumzo ambayo, ghafla, nilifikiria tena mawazo yangu, kwa nikiwa najua kwa kuhofia kwamba labda mambo yamebadilika.

Kwa kweli, ninajiuliza ikiwa bado kuna nafasi ya kushukuru katika enzi ya kujitosheleza na ufanisi, katika jamii kama hii ya sasa, ambapo sheria ya kutaka kupata kila kitu mara moja inatawala, kwa sababu inaonekana kwamba kila kitu kinahitajika, na kwamba hutupa maarifa mkubwa ya kuwa uhuru. Shukrani ni fadhila ya yule ambaye anajua kutambua kuwa anamhitaji mwingine kwa kutambua thamani ya uwepo. Hata katika sala ya Kikristo, shukrani kwa Bwana, kutambua kile tulichonacho kama zawadi tuliyopewa bila malipo kwa sababu ya wema wake, na siyo mastahili ambayo tunaweza kujivunia, utambuzi huu hutuweka katika nafasi sahihi mbele Yake: viumbe mbele ya Muumba.

Kwetu sisi Waabuduo, shukrani, hisia na tunu ambayo katiba huanza, ni ile ambayo inatusukuma kujibu kwa mtindo binafsi upendo mkubwa wa Yesu Msulubiwa, ikitupeleka kwenye kipimo cha uwepo wetu katika huduma kwa watu.



Katika mchakato wa mabadiliko tumeitwa kurejesha tabia ya shukrani ya yule anayeangalia mwingine siyo kama mpinzani, bali kama yule anayethamini maana ya maisha yake.

Kwa hiyo, kukuza moyo wa shukrani kunamaanisha kuendelea kuufanya ubinadamu wetu kukua katika zoezi la Upendo.

*Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC*

## Muhtasari


*Mhariri*
- Upendo ni Shukrani 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Roho ni Uzima 2

*Toka Ulimwengu ASC*
- Yanayoendelea Liberia sasa 3
- Sikukuu ya Bendera 4
- “Mwanamke wa Kihindi” ashinda nafasi ya tatu 5
- “Mwalimu, nifuate” 5
- Ekumenism katika Jimbo letu 6
- Katika Pasaka ya Kristo … Mpango Mzuri wa Vitu 7
- Kwa Kumkumbuka Sista Teresina Vani 8
- Julai 1 – Sikukuu ya Damu Azizi 8
- Ziara ya Kichungaji - Wrocław 9

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- “Shujaa Daima” 10

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 11
- Siku za Kuzaliwa: Tunasherehekea Maisha 11
- Sherehe za Nadhiri za Kitawa 11
- Waliorudi Nyumbani kwa Baba 11

# Roho ni uzima

Tasaufi/roho siyo kitu unachofanywa bali ni jinsi unavyoishi, ni kuwa katika uhusiano, utayari wa kwenda kukutana. Ili kufikia hatua hii ni muhimu kujipanga mwenyewe au kujiunda kulingana na tunu za Yesu. Kama unatamani kufika katika hatua hii ya kuwa, basi, katika maisha ya kiroho, njia maalum au mazoea huhitajika. Kwa mfano, mtu akiwa na hamu ya kuwa mtaalam katika hesabu, kwa hiyo mtu huyo lazima aongozwe na mtaalam mwingine na anahitaji kufanya kazi labda kwa miaka kadhaa kabla ya kupata ujuzi muhimu wa kufanya aina tofauti za hisabati kwa urahisi.

Kupata mtaalam kwa upande wa maisha ya kiroho ni jambo la msingi. Bahati yao wale ambao wamefanikiwa! Wanadamu wote, wakati wa kuumbwa, walipokea msaidizi mwenye ujuzi katika nafsi, Roho Mtakatifu. Kama Wakatoliki tunaanza safari ya maisha ya ufuasi wa Kristo wakati Mungu Utatu Mtaktifu, ambaye tunaamini, humwingiza Roho ndani ya mioyo yetu kwa ubatizo na kutuita kuishi maisha yanayostahili kuwa wanafunzi wakati wa Kipaimara. Kwa hiyo mwenzi / kiongozi bora katika ukuaji wetu wa kiroho ni ROHO MTAKATIFU anayekaa ndani yetu. Mtakatifu Paulo anatukumbusha hili katika barua yake kwa Warumi (8, 15) "Roho ambayo kwa hiyo twalia" "Abba, yaani Baba!" Wakati hatujui namana ya kuomba".

Kwa hivyo swali linalofuata ni: nini cha kufanya ili kuamsha moto wa Roho Mtakatifu? Kila kuamsha au kuangaza huanza na mtu kujifahamu namna alivyo sasa na namna anavyoishi na kwamba anahitaji kubadilika na kuleta matokeo ya kudumu, mabadiliko haya lazima yaanze kutoka ndani. Kwa hiyo tunasikiliza kutoka undani wetu kwa kuzingatia tunu za Injili na kujiuliza: ni kitu gani ndani ya moyo wangu na akili yangu (mawazo na hisia) kinaendana/hakiendani na amri za Yesu (zile mbili muhimu zaidi) ?; Je! ni tabia yangu ipi inaonyesha / haionyeshi tunu za Yesu?

Kwa hatua hii, inaweza kuwa muhimu kuangalia tunu tatu muhimu zaidi ambazo Yesu aliziishi. Kwa maneno mengine, kitu gani tunatarajia kukiishi au tulichonacho kinachofanana na cha Yesu?

kule "KUMTAMBUA BABA "ABBA": kuacha Yesu awe hai ndani na kupitia maisha yetu, kama mama anayeishi katika muungano kamili na mtoto wake, iwe kwa kuwaza mahitaji yake, kicheko, furaha, maumivu, ishara za ukuaji na hata ya harufu yake. Mama hukuza uelewa huu kwa kupanga orodha ya vipaumbele, humweka mtoto kwenye nafazi ya kwanza na kuweka vitu vingine vinavyobaki chini ya orodha, hata mahitaji yake mwenyewe. Hajali tu mahitaji ya mtoto, lakini pia anafurahi na anagundua utekelezaji wake kwa vitendo, hujitambulisha kuwa mama wa mtoto. Kinachofuata ni ukuaji wa uwezo wake wa kuzoea, kuridhika, kutunza kwa upole na kwa uangalifu: yote kwa gharama ya kumfanya mtoto kukua ndani yake, siyo kwa machozi, lakini kwa furaha. Hii inawezekana tu pale ambacho mama hujifananisha na mtoto wake.

Lugha ileile: **lugha ya maneno** ambayo inawasilisha Habari Njema siyo hofu, uhuru siyo amri, faraja siyo lawama, ambayo inaruhusu mwingine kufungua mzigo mzito wa uzoefu wa maisha; **lugha isiyo ya maneno** ya kukubalika bila masharti licha ya udhaifu au mapungufu mengi; **lugha ya kihemko** ambayo inathibitisha mawasiliano ya maneno na yale yasiyo ya maneno na zaidi sana.

Majeraha ya Yesu: Tumeitwa kuishi kwa kuwajali wengine siyo kwa sababu wanatuhitaji sisi, lakini kwa sababu tumeumbwa na tunatamani sana kuendeleza utume wa Yesu katika mazingira ya sasa ambamo tunaishi. Mungu ambaye tunamwamini haishi peke yake, bali anaishi katika umoja na Mwana na Roho, siyo katika nadharia tu bali katika uhalisia. Kuishi na wanadamu wengine wasio wakamilifu mara nyingi husababisha usumbufu. Mara nyingi, katika hali kama hizo, mjaribu hujitokeza na suluhisho rahisi na zinzoonekana kufaa na kupitia njia nyepesi. Tuna mifano kadhaa kutoka katika maisha ya Yesu mwenyewe, kama majaribu matatu jangwani (Lk 4, 1-13); Petro akijaribu kumshawishi Yesu akimbie msalaba (Mk, 8, 32); umati ambao unamtafuta Yesu unamsubiri baada ya muujiza wa mikate ili kumfanya mfalme wao (Yoh 6, 14-15). Katika nyakati hizo zote, kulikuwa na uhusiano wa moja kwa moja kati ya nafsi Utatu ambao ulimfanya Yesu aweze kuchagua njia sahihi, na, mara nyingi, njia sahihi ni ile ya mateso. Kwa hiyo ni vizuri kujiuliza: ninashughulika vipi na watu na hali ambazo zinanifanya kukosa raha? Je! Mimi ninasikiliza kwa makini sauti ya ndani wakati wa kutafuta majibu au suluhisho? Tumruhusu Roho Mtakatifu, aliyemwongoza Yesu jangwani, pia awe kiongozi wetu katika kuishi ***"roho/tasaufi ya Damu ya Kristo".***

***Sr. Bridget Pulickakunnel, ASC***

# Yanayoendelea Liberia sasa

Wiki sita zilizopita, nilifika Grand Cess tu mvua zilipoanza. Usiku uliopita kulikuwa na upepo mkali na mvua kubwa. Kwa mara ya kwanza, mvua iliingia ndani kupitia nyufa za vioo vya madirisha na vyumba viwili vilifurika maji kimojawapo ni kile cha kanisa ndogo ambacho kinatumika kama sakristia tukisubiri kanisa jipya linalojengwa. Kwa kawaida, mvazi na vitu vingine, ambavyo havitumiki vilikuwa kwenye viti na madirisha. Hali hii ilisababisha padri kuja na kufanya maamuzi kuhusu vitu vya kuweka na vya kutupa. Vitu tulivyoweza "kuokoa" tuliviweka kwenye vifurushi juu ya meza ili kivihifadhi vizuri zaidi. Mavazi mengi tuliyokuta yalikuwa yameshonwa kwa sehemu kubwa lakini kamwe hayakuwahi kupindwa na kumalizika. Hii labda ni kwa sababu hapakuwa na yeyote aliyekuwa na sindano na rangi sahihi ya uzi.

Habari njema kwanza. Rais amepitisha mpango kwa ajili ya maskini, na ingawa uchumi ni mbaya (Wakati tulipokuja mwaka jana kiwango cha ubadilishaji kilikuwa dola 135 za Kiliberia kwa dola moja ya US; sasa dola 1 ni 190), anaendeleza miradi kadhaa. Familia ishirini na nne hapa Grand Cess zinzendelea kupoke nyumba ndogo mpya za tofali za saruji zenye paa za bati za zinki (laini kuliko bati zingine). Kazi ilianza mwezi mmoja uliopita ikiwa na wafanyakazi wapatao 25 waliofika kutoka Monrovia. Kama tulivyotarajia, watu hawa wengi katika mji wetu wenye watu 2000 na shughuli hizi nyingi, kumeleta furaha kwa wale wanaopokea nyumba (mawakala wa nje amezunguka mji mzima na kuchagua nyumba zilizokuwa na uhitaji zaidi) . Wiki iliyopita, lori moja la serikali lililobeba mchanga kwa ajili ya kutengeneza matofali ya kuta lilivunja daraja (picha) na kwa wiki moja hapakuwa na gari





iliyofika mjini ila pikipiki ziliweza kuingia na kutoka mjini. Daraja hilo la mbao lililorekebishwa kwa magogo litabadilishwa kwa kujengwa la daraja jipya la chuma hivi karibuni.

Kwa upande wa hali ya shule, kuna ugumu kidogo, kwa sababu baadhi ya wazazi walichelewa sana kulipa ada ya mtihani wa kitaifa, hivyo Wiziri ya Elimu haikuwapa wanafunzi wengi ruhusa ili kufanya mtihani kwa sababu pesa ya mtihani haikufika kwa wakati wizarani. Wanafunzi wetu hawakuruhusiwa kufanya mtihani ambao huwasaidia kuingia katika darasa la 10, mnaweza kuhisi jinsi wazazi na wanafunzi walivyokata tamaa.

Katika wiki nne za kwanza za kipindi hiki cha mwisho, tulikuwa nje ya shule siku 10 kati ya siku 20 za masomo (kipindi hiki tuligawa kadi za rioti za wanafunzi na wazazi walikuja siku moja kati ya siku tatu za mitihani ambapo mvua kubwa iliyonyeesha muda mrefu,). Wiki hiyo, Juni 24-28, tulimaliza mitihani. Hakika kipindi hiki kilikuwa na changamoto. Tulifunga rasmi mwaka wa masomo mnamo Julai 7 kwa ibada ya Misa. Nilijiuliza: "kwa nini wanafunzi wa Shule yetu ya Mt. Patrick hawafanyi vizuri?" Nimejifunza kuruhusu mashaka yangu yapite na kuwa na utulivu kwa sababu mabadiliko yanahitaji muda. Walimu wamehitimu masomo ya juu na wanalipwa karibu $ 40 hadi $ 50 USD kwa mwezi. Wengi wao hufanya vizuri. Nawasikitikia zaidi wanafunzi wale ambao wanataka sana kujifunza na wananyimwa. Najiuliza kwa nini wazazi wanaojitoa sana kulipia masomo ya watoto wao hawalalamiki kama vile wanavyofanya katika nchi yetu.

Tukio lingine lililotokea katika kipindi hiki sehemu nyingine ya Liberia, ni kulazwa kijana mmoja hospitalini hapa akiwa na saratani ndani ya mdomo wake ikijitokeza kutoka shavuni. Alikuwa akifanya kazi ya usafishaji wa madini ya dhahabu (kwa kutumia njia ya kienyeji). Kwa sababu hakuna misaada inayoletolewa na serikali kwa wagonjwa, familia lazima iwajibike kutoa chakula, maji na kulipia dawa. Evelyn, mfanyikazi wa kijamii wa hospitali alikuja kututembele. Sr. Zita alikuwa amemtembelea Frederick na kumsaidia kupata chumba kimoja kwani kijana alikuwa akiugua sana kwa sababu ya saratani ambayo ilisababisha meno yake yaliyokuwa magumu sana kung'oka. Mfanyikazi huyo wa kijamii alitayarisha chakula ambacho Sr. Zita alilipa kwa pesa za zawadi kwa ajili ya Liberia. Federico alifariki baada ya wiki moja na tulimzika hapa. Tulilipia jeneza la kawaida la mbao. Familia yake ni masikini, mama alishafariki na baba ana shinikizo la damu. Federico alimwamini Mungu na, licha ya kuwa alikuwa peke yake bila mwanafamilia, hakubaki peke yake, shukrani kwa Sr. Zita, Evelyn, na wauguzi wengine wenye huruma na upendo kwa kuwa pamoja naye.

Bado kuna mengi ya kusimulia, lakini nafikiri katika hiyo mistari tumewapa ladha la majuma sita ya mwisho. Mvua inanyeesha kila siku, tumekuwa na vikosi viwili vya mchwa weusi wakivamia nyumba na uvamizi wa mchwa wadogo kwenye jokofu letu! Bado hatujajua ni kitu gani kimewavutia.

Kipindi kifupi kilichopita, tulisherehekea Pentekosti tukiwa na wafadhili wa Peace Corps na Padre Francis kwa chakula cha jioni ambacho kilijumuisha keki iliyotengenezwa kwa mchanganyiko maalumu. Tulisherehekea Mwili na Damu ya Kristo na sherehe ya sherehe ya kuzaliwa ya Sr Zita pamoja na ya watoto wawili ambao hufanya kazi kwetu. Siku ya Jumapili, tunapumzika na kufurahia siku.

Sr. Zita anaendelea kufanya kazi mfululizo kwenye madarasa matatu ya ushonaji na kutunza bustani. Tayari tumeshaonja viazi vya kwanza, mihogo, mboga na pilipili kidogo katika milo yetu.

***Sr. Therese Wetta, ASC***

Eneo la Bara: Amerika
Foundation ya Argentina

## Sikukuu ya bendera yetu

Kila mwaka wanafunzi wa kidato cha nne hupaswa kutoa kiapo cha uaminifu kwa bendera ya Argentina, siku ambayo hufanyika kumbukumbu ya kifo cha Jenerali Manuel Belgrano,

mtengenezaji wa bendera yetu ya taifa. Kwa hiyo, mnamo Juni 14, wanafunzi wa kidato cha nne wa mkondo A, walitoa kiapo chao, wakiwa na makamu wa mkuu wa shule hiyo, Bi Silvia Gargaglione kama shahidi wao.

Sherehe hiyo ilifanywa akiwepo Mkuu wa "Jimbo la Armata." Mmoja wa wazazi wa wanafunzi wetu alikuwepo pia, mwanajeshi wa jeshi letu la maji wa Paraguay, na bendi yake, iliyoundwa na watu 30 na yenye aina nyingi za vyombo vya muziki.

Wazazi wa watoto pamoja na Silvia Armesto waliandaa vitafunwa kwa ajili ya wanabendi na wanafunzi. Wote walisherehekea tukio hili kwa shauku na furaha,

Mwishoni watoto walionyesha mchezo na wimbo kwa heshima ya Manuel Belgrano. Wakati wa kupata vitafunwa, Sr. Susana Misermont, ASC aliwakabidhi wanajeshi wa bendi zawadi ya vibebea funguo kwa ajili ya kumbukumbu ya kufika kwa masista wa kwanza Argentina. Wote walishukuru sana kwa uwepo wetu.

Itukuzwe Damu ya Kristo!

***Sr. Susana Misermont, ASC***
*Mwakilishi wa shule*



Region ya USA

## "Mwanamke wa Kihindi" achukua nafasi ya tatu ya ushindi"

Sista Edwina Papa, ambaye anajivunia urithi wake wa kuzaliwa Amerika, aliingiza vipande vitatu vya kazi yake ya sanaa ndani ya Maonyesho ya kwanza ya Eugene Brown Art Show ya 2019 ya kabila la Miami (Myammia) la Miami, Oklahoma. Kazi yake ya "Mwanamke wa kihindi akiwa na simba wa mlimani" aliyoitengeneza kwa kudarisi alama za msalaba kwenye kitambaa cha aida, ilimwezesha kupata zawadi ya medali akiwa mshindi katika nafasi ya tatu.

Aliingiza pia vipande vingine viwili vya sanaa alivyovitengeneza kwa namna tofauti. Farasi aliyechorwa kwa penseli zenye rangi ya maji na mafuta.

Hongera sana, Edwina!

***Sr. Diana Rawlings***








Region ya USA

## "Mwalimu, nifuate"

Hivi karibuni nilikutana na mwanafunzi wangu wa Iraqi, Dunya kwenye sherehe ya maadhimisho ya Eid ambayo inaashiria mwisho wa mwezi wa Ramadhani wa kufunga na sala kwa Waislamu ulimwenguni.

kwenye Sherehe huko St. Louis walitoa chakula na zawadi za bure, pipi mawe, pipi za pamba, rangi za kupaka uso, lori la zima moto na vitu vingine. Wafadhili kutoka, Oasis International, na Kanisa la Baptist la Kanaani walikuwa tayari kusaidia.

Wakimbizi, wahamiaji, na raia wa Amerika walisherehekea kwa utulivu na walifurahi kuwa pamoja. Dunya na rafiki yake Azlar waliongea kwa kiarabu kwa uchangamfu wakati binti zao Sham na Zahraa wakicheza kwenye gari la zima moto. Wakati huo Azlar aliniambia: "Mwalimu, nifuate," wakati akichukua pipi ya jiwe yenye ladha ya limau kwa ajili ya Zahraa.

Maneno hayo yaligusa moyo wangu.

"Mwalimu, nifuate." Wapi, kwa nini, vipi? Tulijiandaa kupita umati wa wanawake wenye mavazi ya hijab waliokuwa wamejitolea kutoa huduma, wakati tukiwa tunasikiliza wimbo wa lugha ambayo sikuelewa.

Maneno haya "Mwalimu, nifuate" yamenisaidia kugundua kuwa nimekuwa nikifanya hivyo kwa zaidi ya miaka miwili tangu nianze kujitolea kwenye Mpango wa kufundisha Wanawake wahamiaji na wakimbizi ambao wanataka kujifunza Kiingereza.

Wanawake hawa wenye ujasiri, na werevu wamenishangaza kwani wanafungua nyumba zao kwa ajili ya darasa la mafunzo ya kila wiki ambalo ni zaidi ya darasa la Kiingereza. Dunya na mimi tulilia pamoja wakati mimba yake ilipoharibika na wakati baba yake huko Baghdad alipofanyiwa upasuaji wa saratani. Tulifurahi pamoja alipopata leseni yake ya udereva ya Marekani.

Yeye hufanya mazoezi ya kuongea Kiingereza lakini mimi sijifunzi Kiarabu. Wengi wetu ambao tunajitolea katika Mpango wa kufundisha Wanawake wahamiaji na Wakimbizi tunashawishika kwamba tunawasaidia wanawake kujifunza Kiingereza tu, lakini kiuhalisia ni zaidi ya hapo. Wanawake daima wanatupeleka kwenye hali mpya ya mahusiano, urafiki, na kubadilishana tamaduni.

"Mwalimu, nifuate."

Ndiyo nitakufuata. Tunatembea pamoja kwa moyo wa huruma wa Mungu. Ni upendeleo gani kwetu na safari gani hii pamoja na wenzi wema namna hii.

***Sr. Regina Siegfried, ASC***





Eneo la Bara: Ulaya
Region ya Italia

# Ekumeni katika Jimbo letu

*Jimbo la Anagni-Alatri -*
*Harakati za Ekumenismu…*
*Katika safari*

Zaidi ya mwaka mmoja uliopita, tukio jipya na la kushangaza lilianza kwenye Jimbo: lile la kujishughulisha kufanya kazi kwa umakini kwa ajili ya umoja na Wakristo wa makanisa mengine. Ilieleweka kuwa kujibu "wito wa ekumeni" ambapo sisi Wakatoliki tumeitwa, haitoshi kujiwekea mipaka tu kwa "Wiki ya sala ya umoja wa Kikristo" ambayo inaadhimishwa kila Januari.

Kwa ujumla, ilikuwa ni lazima kuanza kutoka kwenye jumuiya zetu za parokia, kuhakikisha kila mmoja anajiunda kupitia "wahuishaji wa ekumeni" kwa njia ya kuhimiza mipango zaidi hata kwenye parokia, kwa kukuza mahusiano na Wakristo wa makanisa mengine kuanzia ngazi ya chini na kujihusisha moja kwa moja, na mipango ya jimbo iwezekanavyo.

Kwa hiyo tukio hili mpya lilianza. Sr. Gabriella Grossi, anayehusika kwenye ofisi ya Jimbo kwa ajili ya maswala ya ekumeni, akisaidiwa na tume ndogo aliyoiunda, ameandaa mipango muhimu. Maparoko wote wa parokia za jimbo wanapaswa kuhakikisha kuwa, kila parokia, anapatikana mtu mmoja au wawili ambao wanaweza kuhusika kama "wahuishaji na ekumeni" ili waweze kushiriki katika mafunzo maalum.

Kwa njia hii mikutano saba ya mafunzo ilifanyika (Jumamosi ya kwanza ya kila mwezi kuanzia Desemba 2018) kwenye Kituo cha Kichungaji cha Fiuggi (isipokuwa wa mwisho ambao tulikutana katika nyumba ya Masista Waabuduo Damu ya Kristo huko Anagni).

Wakristo kadhaa wa Waaldensia kutoka Anagni na Ferentino, ambao walialikwa na Paroko wa Tufano Padre Marcello Coretti, walihudhuria pia mikutano hii. Urafiki na uhusiano wa pande zote mara moja ulizaliwa ambao uliimarisha uhusiano miongoni mwao.

Kwa kweli hatua hizi za mwanzo zilichochea zaidi mang'amuzi ya "Wiki ya sala kwa ajili ya umoja wa Wakristo" ambayo iliadhimishwa, kwa mara ya kwanza, katika Kanisa kuu la Anagni, akiwepo Askofu wetu Lorenzo na wachungaji wa Kanisa la Methodist Valdese la Ferentino na la kanisa la Rumeno-Orthodox la Alatri. Mazingira mazuri ya kufahamiana wakati wa maadhimisho na pia, baadaye, katika makaribisho ya kindugu yaliyofuata.

Lakini mipango mingine ya ekumeni imeonyesha mwaka huu wa kwanza wa shughuli zifuatazo:

- mnamo Machi 10, baadhi ya kundi la wahuishaji walioshiriki kwenye sala ya kiulimwengu iliyoandaliwa na wanawake wa Waaldensia wa Slovenia mwaka huu; huko Ferentino, katika Kanisa la Waldensia,
- Mei 18, kikundi kilishiriki katika ibada ya hija ya kiekumeni huko Roma, walitembelea makanisa muhimu zaidi ya Kikristo katika mji huo mkuu;
- Kila mwezi Mei wanandoa wetu mojawapo hushiriki katika "Kituo cha Ekumeni" huko Velletri kwa ajili ya siku ya sala;
- Mwishowe, mnamo tarehe 9 Juni huko Anagni, kwenye hafla ya maonyesho ya "Sikukuu ya Watu", Tume ya Kiekumeni iliandaa kipindi kifupi cha sala ya umoja wa dini kabla ya sherehe ya onyesho la aina za bidhaa kutoka ulimwenguni.

Mwishoni mwa mkutano wa mwisho wa mwezi tuliachana kwa nia ya kuanza tena huu uzoefu mzuri, kwa baraka na maneno ya kutia moyo ya Askofu wetu Lorenzo.

***Gianni Rontani***
***Mjumbe wa Tume***
***rasmi kwa ajili ya Ekumeni ya Jimbo***



# Katika Pasaka ya Kristo…Mpango mzuri wa vitu

*Taarifa ya mkutano*



Mji wa Orvieto (Terni) kwenye Kanisa lake Kuu la Jimbo kuna masalia ya Damu ya Kristo kutoka kwenye hostia ambayo iligeuzwa na Padre Petro kwenye karne ya 13.

Fumbo la Agano Jipya ambalo Kristo alilifanya kwa Damu yake na ambalo hulifanya upya katika kila adhimisho la Misa Takatifu, lilithibitishwa katika mwili huo unaotolewa kwa karne nyingi, na hupewa sifa na kuabudiwa na waumini kila siku.

Kwa sababu hiyo, Sr. Anna Maria Vissani na Wanachama wengine wa eneo hilo, Sr. Gabriella Grossi, Sr. Maria Paniccia na Sr. Grazia Cafaro waliamua kupanga mkutano kwa ajili ya marafiki zetu na wanachama kwenye jumuiya ASC huko Orvieto.

Jumapili, tarehe 2 Juni, karibu watu sabini, wakiwemo masista ASC, Walei na mapadre, walikusanyika kwenye chumba kikubwa cha chakula cha "Mtakatifu Paulo" kwa ajili ya tafakari ya fumbo la uumbaji na ukombozi.

Baada ya kifungua kinywa kizuri kilichotolewa kwa wote waliofika, Sr. Anna Maria alitoa utangulizi wa siku akiwasilisha mpango na lengo. Mkuu wa Region Sr. Nicla Spezzati, katika mazungumzo yake, alikazia muunganiko uliopo kati ya Furaha ya Injili kama inavyoelezwa na Papa Francisco katika kitabu cha Furaha ya Injili na uelewa wetu kama watawa na walei kuhusu kutiwa muhuri na kukombolewa kwa Damu ya Kristo.



Ulifuata usomaji wa matini iliyoandaliwa kwa umakini, dansi ya uumbaji, iliyoandaliwa na Kituo cha Kiroho cha Castelplanio na kusikiliza mapigo ya kinanda kilichopigwa na Sr. Maria Pia De Fins, ASC.

Mwonekana wa picha nzuri za uumbaji kwenye projector ziliwafanya washiriki kuingia kwa kina katika maana ya somo, utenzi wa uzuri wa kazi ya uumbaji wa Mungu na kwenye tumaini la ukombozi ambao hata viumbe vinausubiri. Sr. Maria Pia alifungua na kufunga fumbo lake la somo la mziki wa Asubuhi wa Edward Grieg na alichangia kuwaingiza washiriki katika hali nzuri ya tafakari.

Wakati wa mapumziko, kwenye mazingira ya kuvutia ya uwa wa nyumba ya watawa wenye kisima cha kale katikati, kijana Amanda, mwanafunzi wa shule ya mafunzo ya kupiga filimbi aliipiga vizuri kwa muda na kuzima sauti za watu ambao walikuwa wanafurahia muda wa kipupwe ambao ulikuwa umewadia.



Katika adhimisho la Misa lililoongozwa na Padre Marino Piccotti, anayefanya kazi kwenye Kituo cha Kiroho na Paroko wa Castelplanio, aliadhimisha sikukuu ya Kupaa Bwana akiwaalika washiriki wote kuamini kweli kuwa Yesu, alipokuwa anapaa mbinguni alituachia Roho wake abaki nasi na kutuachia mwili wake na damu yake.

Katika muda huru tulipita katika barabara za kati za mji na tulijikuta wote mbele ya tao zuri la Kanisa Kuu la jimbo. Sr. Patrizia Pasquini, ASC alitueleza sehemu muhimu za jengo na za sanamu za nakshi za karne ya kumi na tatu na kisha alieleza kwa kina sehemu ya ndani ya kanisa la Mwili. Tuliingia kanisani katika hali ya ukimya na kubaki kwa muda katika sala mbele ya altare ya muujiza tukimaliza kwa utenzi Enyi Watu wote pigeni makofi, tukisindikizwa na kinanda cha Sr. Maria Pia.

Siku ilimalizika kwa kutembela kanisa jipya, lililonaksiwa na Beato Angelico na Luca Signorelli. Ndani yake fumbo la uovu ambalo linakumbatia karne limeshindwa na nguvu ya Kristo ambaye anawarudishia wanadamu heshima kamili ya wana wa Mungu.

Muda wa siku hiyo uliacha katika mioyo ya wote wito wa kuzama kwa kina katika Fumbo la Pasaka la Kristo ambalo ni kiini na msingi wa karama ya Waabuduo Damu ya Kristo.

***Waabuduo Damu ya Kristo - Castelplanio***

Region ya Italia

# Kwa Kumkumbuka Sista Teresina Vani

Napoli, 20 Juni 2019

Mheshimiwa Mama Mkuu,

Ninapenda kutoa shukrani za dhati kwako na kwa masista wako wema sana kwa kumjali na kumpa mtatunzo mazuri yenye upendo Sista Teresina wakati wa ugonjwa wake, na pia kwa moyo wa upendo ambao mlituonenyesha mlipotukaribisha sisi sote.

Zaidi sana, wakati wa ibada ya mazishi, tulijikuta katika mazingira ya upendo, utulivu, amani na faraja ya kibinadamu na ya kiroho kiasi kwamba kwa wakati huo hatukugubikwa na huzuni. Sote tulikuwa tukijua kuwa, Sista Teresina, mwishoni mwa maisha ya kujitoa kabisa kwa Bwana alikuwa ameiacha "Jumamosi" kwa tabasamu usoni mwake na kuingia kwenye furaha ya "sikukuu isiyo na mwisho", kama ilivyoandikwa kwenye wasifu wake mzuri ambao mlituzawadia.

Kwa hayo yote tunawajibu wa kuwashukuru ninyi nyote na kwa namna ya pekee, mheshimiwa Mama.

Kwa hayo; ninawashukuru, na kuwasalimu kwa kumbatio la shukrani.

***Orazio Vani***



Region ya Wrocław

# Julai 1 – Sikukuu ya Damu Azizi

Damu ya Kristo, bila hiyo hakuna msamaha: hii ilikuwa ni sala ya litania ambalo mwaka huu askofu Marek Mendyk alitaka kuifafanua na kuielezea kwa kina wakati wa mahubiri ya Adhimisho la Misa ya tarehe 1 Julai huko Bolesławiec. Tumeitwa ili tuwe wajumbe wa upatanisho ili kuleta amani kwa wengine. Hii inawezekana ikiwa katika maisha yetu tuna amani na upatanisho ambao hutokanana na Damu ya Kristo.



Kwa miaka mingi Askofu Marek, huko Bolesławiec, huongoza Adhimisho la Misa kwa heshima ya Damu ya Kristo ambayo tunaisherehekea pamoja na wanachama, ambao wanaishi tasaufi ya Damu ya Kristo wakimfuata Yesu katika maisha ya kila siku. Uchaguzi wa safari hii unakuwa ni mtindo wa maisha, ukitoa uelewa kwa kiasi kikubwa wa misalaba ya kila siku tunayokutana nayo.

Katika sikukuu ya Damu ya Kristo , tulisimama kukumbuka ukweli wa upendo wa Mungu kwa kila mmoja wetu. Kama tunafahamu ukweli huu, tunaelewa, tunaonja uponyaji wa kweli na uhuru wa ndani.

Tunamshukuru Mungu kwa ajili ya Wanachama wengi wa Damu ya Kristo wa Bolesławiec na wa maeneo jirani ambao walishirikishana nasi furaha ya adhimisho, ambapo ulifuata mchezo wa kikundi cha ngoma cha Bolesławiec. Neema ya Mungu ni kuu na katika majeraha yake tunapata uponyaji wetu.

***Sr. Ewa Kleps, ASC***

# Ziara ya Kichungaji – Wrocław

***"Mioyo ... katika Umoja: Injili Ulimwengu"***

Hii ilikuwa ni mada ya ziara ya kichungaji ya Uongozi Mkuu ambayo ilifanyika kwenye Region yetu kuanzia tarehe 21 Mei hadi 14 Juni 2019. Mada hii iliwasindikiza masista wa Region nzima wakati wa mikutano pamoja na Dada zetu wa Uongozi Mkuu. Mikutano ilifanyika kwa siku tatu, ambapo moja ulifanyika huko Bolesławiec na miwili huko Częstochowa. Lengo la ziara lilionyesha dira ya Shirika letu kwa wakati ujao. Kwenye barua ya Ubainisho ya Hati ya Mkutano Mkuu wa 2017 kuna mwaliko wa kufanya mabadiliko. Sisi sote ndani ya Shirika tuko pamoja kwenye mchakato wa mabadiliko. Roho anatuhimiza kujenga umoja. Sisi kama Shirika tunajisikia kuitwa kuwa ishara ya umoja, ushirika katika ulimwengu na hii ni Injili. Ulimwengu wa leo unahitaji mifano ya kweli ya Injili. Ulimwengu unataka kuona kuwa tunafanya yote kwa ajili ya kuishi katika ushirika. Hamu ya Yesu ni huu umoja ambao Mtakatifu Paulo anauandika katika barua kwa Wafilipi (2, 2-5). Umoja humaanisha maisha bila kujipendelea, ubinafsi na mashindano... bila kutafuta faida binafsi, bali kutaka faida na furaha kwa ajili ya wengine. Hii hamu ya kutaka kuwa katika umoja inaweza kufikiwa tu kupitia mabadiliko ambayo yanaanza na mimi mwenyewe katika jumuiya ambayo kwetu sisi ni zawadi, lakini pia ni wajibu. Wajibu wetu ni kukua kama wanafunzi wa Yesu ili kufikia lengo la utakatifu.

Kwa kuzingatia tunu za maisha ya kijumuiya tunapaswa daima kutoa nafasi ya kwanza kwa ajili msamaha na upatanisho na kusaidiana katika kujenga hali ya amani na furaha. Kwa njia hii jumuiya itakuwa mahali pa faraja ambapo tunaonja uzuri wa njili, wa maisha ya mahusiano ya mtu na mtu, utamu na upendo ambao hupomya majeraha yetu. Tunapaswa kukumbuka kazi endelevu kibinafsi, kijumuiya, kiregion na kishirika. Wakati wa kazi za vikundi na mashirikisho tulionyesha njia muhimu za kujenga umoja wa kweli ambao Yesu anautaka. Yeye alitoa maisha yake kwa ajili ya umoja. Sisi tunapaswa kutaka kwa nguvu, kutunza mahusiano mazuri, tunapaswa kuwa na mioyo wazi na muda kwa ajili ya wengine, kuishi katika ushirika ili kuwa Injili katika ulimwengu. Tutatadhimini dhima yetu na mpango wetu wa maisha katika jumuiya mara kwa mara: namna yetu ya kuhudumia, namna ya kumshuhudia Yesu, tukikumbuka kuwa huduma ni upendo. Katika shughuli zetu zote na katika mchakato wa mabadiliko tunasindikizwa na upendo wa Mungu Baba kwa njia ya Yesu katika Roho Mtakatifu.

Kwa imani katika nguvu ya Damu ya Krsito

***Sr. Bernadetta Pajdzik, ASC***





# "Shujaa Daima"



Shule inawakilisha mahali penye upendeleo na mahali maalum pa kuendeleza utaratibu na mikakati iliyoundwa kukuza uvumbuzi na upendo kwa mazingira, kuamsha hitaji la mazingira safi na uhusiano mzuri na yenye kujenga kwa kuheshimu sheria, pia kupitia kusoma na kufanya maonyesho ya hadithi.

Kwa lengo hili, hata mwaka huu, licha ya kustaafu kazi ya kufundisha, nilikuwa na furaha ya kurudi kuendelea kutafuta misaada kwa ajili ya Mradi wenye sehemu nyingi wa "Maremetamare na hadithi za Wimbi" za Fedele Eugenio Boffoli na Paride A. Cabas ulioandaliwa na mwalimu Floriana Massa na wanafunzi wa IV F - wa kutwa wa shule ya IC Dante-Galiani, kwa usahihi na umakini mkubwa kwa mazingira, kupitia hadithi ya "shujaa milele" na kushiriki katika mwendelezo wake.

Katika utekelezaji wa Mradi, mang'amuzi ya kisanii yalitumika ili kutoa mwongozo kwa muda na nafasi kwa tunu endelevu ya maisha, mazingira, usahihi na ushirikiano. Pamoja na mradi huu ilikusudiwa kuendelea kuwaingiza watoto kwenye mada ya mazingira, elimu ya viumbe na mimea na haki; kuwawezesha kuelewa hitaji la kutambua na kukuza kila siku tabia za kusaidiana na zenye kujali afya na zisizobagua mahusiano. Haya yalikuwa ni malengo ya mchakato wa "Maendeleo na Elimu kwa ajili ya kulinda bahari, chanzo cha uhai" ambao tayari ulishaanza kutekelezwa miaka iliyopita kwa umakini wa pekee kwenye mada ya haki na utunzaji wa "nyumba yetu ya pamoja" ambayo hutuhifadhi.

Watoto walisaidiwa kujenga mahusiano ya kiutu katika mwingiliano wa tamaduni na kushinda dhana potofu. Kupitia ujuzi wa maisha ya ushuhuda wa haki wa wafiadini kama G. Falcone, P. Borsellino, Padre Peppe Diana, Lqbal Masih, Bakhita n.k, tafakari zilielekezwa kwenye umuhimu wa maadili ya tabia sahihi ili kumfanya kila mtu kuishi kwa amani maisha ya pamoja yanayoashiriwa na uwepo wa tunu za usawa, uhuru, haki, uhakika na heshima kwa kila kitu na kwa kila mtu.



Pamoja na hayo tumetafuta kujenga maana ya haki ili kuendeleza tabia ya uwajibikaji. Watoto waliwezeshwa kushikamana na mazingira yanayowazunguka, hivyo, waliweza kuzoea kutenga muda mara kwa mara ili kuweza kuyatunza – kwa kuyasafisha, kuhifadhi taka kwa kuzibadilisha zifae kwa matumizi mengine, kumwagilia, kupanda maua na mti mmoja wa mzeituni kwenye bustani yao ya shule na kuendeleza kwa kina maana ya "haki";

watoto wadogo waliunda herufi za haki, walizifanya kwa mtindo wa kisanii na walisaidiwa kujifunza na kuiheshimu mazingira. Kupitia mkutano na mwandishi wa hadithi na maonyesho ya mwisho, watoto waliweza kupata fursa ya kushirikishana na familia zao kile walichojifunza.

***"Katika kila kipengele cha maisha huwepo kitu kilicho kinyume katika kila moyo wa haramia kama ilivyo katika kitu kingine chochote."*** (Fedele Boffoli)

Ni hadithi ya mfano wa ukombozi wa haramia ambaye – alipanda melini ili kumwokoa mtumishi wake kijana ambaye alikuwa apigwe risasi, alijiingiza kwenye mapambano kati ya kijana na mshambulizi wake, akaishia kujeruhiwa na kutumbukia majini na meli ilivunjika, alijishikilia ndani ya kasha na hatimaye kujikuta kwenye kisiwa cha ajabu cha Sesta Rega ambako kila mtu huishi kwa amani, akila matunda ya nchi na ya kazi zao, bila kutaka kumiliki vitu, wakisaidiana kila mmoja na kuheshimu mazingira. Hili ni fundisho muhimu ambalo ni kinyume na sera za unyonyaji za dunia na rasilimali watu ambazo hutumiwa isivyohalali. Fundisho hili linapaswa kutekelezwa kinadharia na kivitendo na watoto kupitia njia mbalimbali (kusoma, kusikiliza, kutafsiri, na kujenga kupitia sanaa na miundo mbalimbali) ili hupata matokeo yake muhimu yanayoonekana siku ya mwisho.

Kutoka katika tafakari ya mzazi mmoja (L. Varano):

*"Tuna uhakika kuwa mchakato huu wa malezi utakuwa kwa vijana wetu njia ya kuwa na tumaini la kuwa wenyeji huru kiasi cha kuweza kutoa maamuzi binafsi na kutambua yale yasiyosahihi, lakini pia kuangalia kwa matumaini wakati ujao katika kulinda na kutunza "Nyumba yetu ya pamoja" ambayo hutuhifadhi. Tunashukuru sana kwa haya yote."*

***Sr. Rosalba Facecchia, ASC***

## Kalenda ya Uongozi Mkuu

**4 Septemba:** Jumuiya ya malezi kuhamia kwenye makao ya Novisiati ya Shirika huko via G. Gatti, 13 - 00164 Roma
**6-8 Septemba:** Sr. Nadia Coppa na Sr. Bridget Pulickakunnel watakuwa kwenye ziara ya kichungaji huko Hispania
**10-23 Septemba:** Sr. Dani Brought na Sr. Maria Grazia Boccamazzo watakuwa Tanzania kwa ajili ya kushiriki adhimisho la jubilei ya miaka 50 tangu kufika ASC Manyoni
**23-28 Septemba:** Sr. Bridget Pulickakunnel atakutana na Tume ya Marekebisho ya Sheria halisi za Shirika.

## Siku za kuzaliwa: Tunasherehekea Maisha ya

| | | |
|---|---|---|
| miaka 40 | | |
| **Sr. Ljilja Muzić** | 23/09/1979 | Zagabria |
| miaka 50 | | |
| **Sr. Mara Župarić** | 04/09/1969 | Zagabria |
| miaka 60 | | |
| **Sr. Vianeja Čolić** | 12/09/1959 | Zagabria |
| miaka 70 | | |
| **Sr. Branislava Garvan** | 26/09/1949 | Zagabria |
| **Sr. Marisa Daniele** | 28/09/1949 | Italia |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Rosaria Salvemini** | 15/09/1939 | Italia |
| **Sr. Teresina Veronese** | 13/09/1939 | Italia |

## Waliorudi Nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 17/07/2019 | **Sr. Agnese (Angela) Bianchi** | Italia |
| 24/07/2019 | **Sr. Lisbeth Reichlin** | Schaan |
| 24/08/2019 | **Sr. Michelina Sebastiano** | Italia |


Gazeti la Kimataifa
Waabuduo Damu ya Kristo
...Kwa Neno Lako...

**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 8, Septemba 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*


## Sherehe za Nadhiri za kitawa

### 8 Septemba 2019

**Miaka 60 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Zagabria**
*Sr. Marija Ćosić*

**Miaka 60 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Schaan**
*Sr. Mathild Frick*

### 12 Septemba 2019

**Miaka 25 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Italia**
*Sr. Carmela De Michele*
*Sr. Maria Chiara Maselli*

**Miaka 50 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Italia**
*Sr. Grazia Cafaro*
*Sr. Marisa Daniele*
*Sr. Maria Pia Iadanza*
*Sr. Carolina (Carla) Poppa*
*Sr. Nicla Spezzati*

**Miaka 60 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Zagabria**
*Sr. Antonietta Petrosino*

### 15 Septemba 2019

**Nadhiri za Kwanza za Kitawa - Region ya Zagabria**
*Kristina Vuković*
*Ivana Milićević*

**Miaka 25 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Tanzania**
*Sr. Josephina Paul*

**Miaka 60 ya Nadhiri za Kitawa - Region ya Wrocław**
*Sr. Urszula Droszczak*
*Sr. Marta Jurasik*
*Sr. Anieli Mroczek*
*Sr. Janina Sygut*
*Sr. Imelda Sygut*

**Miaka 60 na 65 ya Nadhiri za Kitawa - Ruma Center**
*Sr. Gabrielle Rowe (60°)*
*Sr. Genarose Buechler (65°)*
*Sr. Ann Frances Gross (65°)*
*Sr. Rose Anthony Mathews (65°)*
*Sr. Mary Louise Degenhart (65°)*

**Miaka 70 na 75 ya Nadhiri za Kitawa - Ruma Center**
*Sr. Elizabeth Kolmer (70°)*
*Sr. Helen Kiefer (70°)*
*Sr. Mary Rachel Lawler (70°)*
*Sr. Irene McGrath (75°)*
*Sr. Mary Ann Mueller (75°)*